Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1371

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 6, Issue 1, 2023
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Kuchambua Mbinu za Kiaristotle na Zisizo za Kiaristotle katika Tamthiliya ya Sadaka ya John Okello

*Emmanuel Oscar Msangi*[1*]

[1] Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, S. L. P. 23409 Dar es Salaam, Tanzania.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: emmanuel.msangi@out.ac.tz

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1371**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*13 Agosti 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Sadaka, Tanzia, Dayolojia, Mbinu, Nathari, Sampuli, Tasnia, Drama.*

**IKISIRI**

Uandishi wa tamthiliya kwa mwega wa Kiaristotle umekuwa na athari kubwa sana kwa waandishi wa Kiafrika. Katika fasihi ya Kiswahili, baadhi ya waandishi wa mwanzo walioathiriwa na mkabala huo ni Ebrahim Hussein na Penina Mlama (Wafula na wenzake, 2020). Makala haya yanachambua mbinu za Kiaristotle na zisizo za Kiaristotle katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* (Mbogo, 2015). Mbinu ya usomaji makini ndiyo imetumiwa kukusanya data. Data zimewasilishwa kwa Mkabala wa Kimaelezo. Ukusanyaji, uchambuzi na mjadala katika makala haya umeongozwa na Nadharia ya Kiaristotle. Kimsingi, Emmanuel Mbogo, mtunzi teule ametumia mbinu za Kiaristotle na zisizo za Kiaristotle katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* (2015). Mbinu za Kiaristotle zimejidhihirisha kupitia vipengele vya msuko, wahusika, lugha za kishairi, uteuzi wa misamiati, na dhamira. Mbinu zisizo za Kiaristotle zimejidhihirisha kupitia mbinu za monolojia, kuchanganya nathari na ushairi, pamoja na dayalojia. Makala haya yanaeleza kuwa tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* ni drama tanzia. Drama hii imebeba sifa nyingi za Kiaristotle na sifa chache zisizo za Kiaristotle. Mhusika mkuu John Okello amepitia mambo mazito na magumu ambayo mtu yeyote akikutana na kazi hii lazima ahisi huzuni moyoni mwake na amwonee mhusika huyu huruma kwa mateso na malipo mabaya aliyoyapata. Kutokana na mikondo mbalimbali ambayo drama tanzia inapitia si lazima tena shujaa au mhusika mkuu atoke familia ya tabaka la juu au tabaka tawala. Mhusika mkuu sasa anaweza kutoka tabaka lolote katika jamii yoyote.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1371

**APA CITATION**

Msangi, E. O. (2023). Kuchambua Mbinu za Kiaristotle na Zisizo za Kiaristotle katika Tamthiliya ya Sadaka ya John Okello *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 259-273. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1371.

**CHICAGO CITATION**

Msangi, Emmanuel Oscar. 2023. "Kuchambua Mbinu za Kiaristotle na Zisizo za Kiaristotle katika Tamthiliya ya Sadaka ya John Okello". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 259-273. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1371.

**HARVARD CITATION**

Msangi, E. O. (2023) "Kuchambua Mbinu za Kiaristotle na Zisizo za Kiaristotle katika Tamthiliya ya Sadaka ya John Okello", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 259-273. doi: 10.37284/jammk.6.1.1371.

**IEEE CITATION**

E. O., Msangi, "Kuchambua Mbinu za Kiaristotle na Zisizo za Kiaristotle katika Tamthiliya ya Sadaka ya John Okello", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 259-273, Aug. 2023.

**MLA CITATION**

Msangi, Emmanuel Oscar. "Kuchambua Mbinu za Kiaristotle na Zisizo za Kiaristotle katika Tamthiliya ya Sadaka ya John Okello". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Aug. 2023, pp. 259-273, doi:10.37284/jammk.6.1.1371.

## UTANGULIZI

Watafiti mbalimbali wamefanya tafiti katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* mathalani Awhida (2021), Omar (2019) na Msangi (2018). Kila mtafiti amechunguza tamthiliya hiyo kutokana na malengo ya utafiti wake. Lengo la makala haya lilikuwa kuchunguza mbinu za kiaristotle na zisizo za kiaristotle katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello*. Mtafiti alinia kuchambua mbinu za kiaristotle na zisizo za kiaristotle katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* kwani tafiti tangulizi zote, hazikushughulika na mada hii. Nadharia ya Kiaristotle ndiyo ilituongoza kufanya uchambuzi huu. Nadharia hiyo ilikuwa muafaka kwetu kwani ni nadharia inayotazama zaidi sifa msingi za tamthiliya tanzia.

Emmanuel Mbogo, mwandishi wa tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* ametumia mbinu za kiaristotle katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello*. Hata hivyo kutokana na maendeleo ya tasnia ya tamthiliya, tamthiliya tanzia zama hizi zinahusisha mbinu nyingine zaidi ya pale alipoishia Aristotle. Mathalani mhusika mkuu zama hizi katika tanzia si lazima atoke tabaka tawala, la juu, la nasaba bora. Katika makala haya tumenuia kuchambua mbinu za kiaristotle na zisizo za kiaristotle zilizotumika katika tamthiliya teule. Uchambuzi wa mbinu mbalimbali za kiaristotle umeegemea katika mihimili ya nadharia ya kiaristotle. Katika sehemu inayofuata tumefasili dhana za msingi zinazorejewa katika makala haya.

## FASILI YA DRAMA, TAMTHILIYA NA TANZIA

Wamitila (2008) anasema, "Drama ni dhana inayorejelea kazi ya fasihi iliyoandikwa kwa ajili ya kuwasilishwa jukwaani kwa njia ya maneno na ishara." Mwanazuoni huyu anazidi kueleza kuwa drama inaweza kutofautishwa kwa vigezo mbalimbali. Mathalani idadi ya matendo (drama ya tendo moja, drama ya matendo mawili n.k), idadi ya waigizaji (mono drama - drama ya mwigizaji mmoja, duo drama – drama ya waigizaji wawili), kiwango cha utegemeaji wa muziki, mtindo wa msuko wake (tanzia, futuhi, tanzia – futuhi n.k.), maudhui yake (kichekesho, maadili, tatizo).

Chimerah na Njogu (2011) wanafasili tamthiliya kama tawi la fasihi andishi linalohusu maigizo ya maisha halisi ya binadamu, na mambo yanayomshughulisha katika maisha hayo. Maigizo hayo hujumuisha jukwaa (pahala pa kuigizia), mazungumzo ya wahusika, maleba au mavazi ya wahusika, vifaa vya kuigizia, jinsi ya kuigiza n.k. Hali kadhalika kupitia wanazuoni hawa tunabaini kuwa tamthiliya hujengwa katika maonyesho mbalimbali yanayokamilisha. Watunzi wa tamthiliya hupanga maonyesho hayo kwa namna inayowafaa kufikisha ujumbe waliokusudia kwa hadhira lengwa.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

Mulokozi (2017) anasema, “tamthiliya au drama ni igizo la kisanaa lilikusudiwa kutendwa jukwaani kwa ajili ya hadhira fulani. Hivyo kwa kawaida tamthiliya huitwa mchezo wa kuigiza.” Mwanazuoni huyu anaendelea kueleza kuwa tamthiliya inaweza kuwa imeandikwa au kutoandikwa. Hali kadhalika tamthiliya hujengwa katika masimulizi ya pande mbili zinazogongana. Mgongano huo ndiyo huwa kiini cha tamthiliya na unaposuluhishwa ndipo tamthiliya humalizika.

Kimsingi, dhana za drama na tamthiliya zinahusu sanaa za maonyesho. Wanazuoni tuliopitia hapo juu Wamitila (2010), Chimerah na Njogu (2011) na Mulokozi (2017) wanafasili tamthiliya au drama kama kazi za fasihi ambazo usanii na utendaji wake hutegemea zaidi vitendo na uongeaji mbele ya hadhira. Hata hivyo wanazuoni hawa wanakubaliana kwamba tamthiliya inaweza kusomwa pekee, isichezwe jukwaani. Tamthiliya hiyo inapochezwa jukwaani ndipo huitwa drama. Wamitila (2008) ameeleza kuwa drama inajikitiza zaidi kwenye kazi ya fasihi iliyoandikwa ili iigizwe jukwaani kwa njia ya maneno au ishara. Igizo mbele ya hadhira katika jukwaa ndiyo sifa kuu ya kuieleza dhana ya drama. Utanzu wa tamthiliya unaelezwa kama tawi la sanaa za maonyesho ambalo halisisitizi zaidi suala la uigizaji jukwaani. Kwa vile drama na tamthiliya ni sanaa za maonyesho basi huwa na sifa msingi zinazoitambulisha. Mhando & Balisidya (1976, uk. 4) wanabainisha sifa msingi za tamthiliya. Sifa hizo ni: Dhana inayotendeka; Mtendaji; Uwanja wa kutendea na Watazamaji.

Tamthiliya uainishwa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali mathalani kigezo cha muda unaotumika kuicheza na kigezo cha maudhui yaliyomo ndani yake (Omar, 2020). Kupitia mihadhara ya tamthiliya ya Kiswahili aliyowasilisha Omar (ktj) tunabaini kwamba tunaweza kuvitumia vigezo vya muda (duration) na utanzu (genre) kuzigawa tamthiliya katika aina mbalimbali. Kwa mujibu wa kigezo cha kwanza, muda, kuna tamthiliya ambazo huwa na tendo moja na huchukua muda mfupi. Tamthiliya yenye maonyesho mengi huchukua muda mwingi. Kigezo cha muda hutegemea wakati unaotumika kucheza tamthiliya hiyo. Kigezo cha utanzu hutegemea yaliyomo (maudhui) au mada ya tamthiliya mahsusi. Kutokana na kigezo hiki cha pili tunaweza kuainisha tamthiliya katika aina zifuatazo:

- Tanzia (Tragedy Play)
- Futuhi/Komedia (Comedy Play)
- Melodrama (Melodrama Play)
- Kichekesho (Farce Play)
- Tanzia–ramsa/Tanzia-futuhi (Tragicomedy Play)
- Tamthiliya ya Kihistoria (Historical Play)
- Tamthiliya Tatizo (Problem Play)
- Tamthiliya ya Kibwege (Absurd Drama)

Katika makala haya tumechunguza tamthiliya tanzia. Tanzia ni aina ya tamthiliya yenye uzito unaodhihirika kihisia au kififkra (Wafula na wenzake). Wanazuoni hao wanaendelea kueleza kuwa tamthiliya tanzia huwa na suala, matendo na malengo dhati. Tamthiliya hiyo inapoigizwa mbele ya hadhira huibua hisia za hofu kwa hadhira wanaotazama au kuisoma (Mahenge, 2016).

Kimsingi, tanzia ni tamthiliya yenye huzuni ambayo inagusa hisia za watazamaji kiasi cha kuogopesha na kumwonea huruma mhusika mkuu ambaye hupata janga. Mara zote huyo mhusika mkuu huwa na mwenendo bora unaokubalika na jamii. Pia mhusika huyo huwa mwenye msimamo. Janga analopata mhusika mkuu linapaswa lisiwe kubwa kiasi cha kusababisha mtazamaji kuogopa sana hata kushindwa kumwonea huruma mhusika (Wamitila, 2003).

## MBINU ZA UTAFITI NA NADHARIA YA UCHAMBUZI

Katika sehemu hii tumeeleza mbinu zilizotumika kukusanya data, sampuli na usampulishaji hatmaye tukaeleza nadhari iliyotumika kuchambua data.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

Mbinu ya usomaji makini imetumika kusoma tamthiliya teule, *Sadaka ya John Okello*. Mkabala wa kimaelezo umetumika kuchambua za utafiti. Nadharia ya kiaristotle ndiyo ilituongoza kukusanya data na kuchambua data katika makala haya. Katika sehemu inayofuata tumeeleza vipengele hivi kwa undani.

**Mbinu ya Usomaji Makini**

Mbinu ya usomaji makini ndiyo ilitumika kukusanya data za makala haya katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* na machapisho mbalimbali maktaba na mtandaoni. Zelda (2022) anaeleza mbinu ya usomaji makini kama mbinu inayotumika kutafuta data za utafiti katika machapisho mbalimbali mathalani vitabu, majarida, tahakiki n.k. Mtafiti husoma machapisho hayo ili kupata data zitakazofanikisha malengo ya utafiti anaofanya. Wanazuoni wengine wanaitambulisha mbinu hii kama mbinu ya usomaji maktabani (Ochieng, 2020). Mtafiti hupata machapisho hayo katika maktaba, maduka ya vitabu ama mtandaoni katika vyanzo mbalimbali huria vinavyotolewa na taasisi mbalimbali za kitaaluma.

**Usampulishaji**

Sampuli ya makala haya ilitokana na usampulishaji lengwa. Usampulishaji lengwa ni mchakato unaotoa fursa kwa mtafiti kuchagua sampuli ambayo inaendana zaidi na lengo la utafiti anaofanya (Ponera, 2019). Sampuli inayoteuliwa huwa na nafasi kubwa ya kutoa data dhidi ya utafiti unaofanyika. Katika mbinu hii ya usampulishaji lengwa mtafiti huchagua sampuli ya utafiti akizingatia zaidi ukubwa wa data atakayopataka katika sampuli hiyo. Katika makala haya tulitumia mbinu hii kuteua sampuli ya tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* kwani ilikuwa na nafasi kubwa ya kufanikisha lengo la makala tuliyokuwa tunaandika.

**Nadharia ya Kiaristotle**

Nadharia ya Kiaristotle iliasisiwa na Aristotle, Myunani kutoka huko Ulaya (Mbogo, 2016). Nadharia hii hutumika kuhakiki tamthiliya za Kiswahili, mathalani miundo ya tamthiliya tanzia. **Aristotle** alikuwa mwanafalsafa muhimu sana wa ustaarabu wa Ugiriki ya kale (Hunt, 2021). Kupitia andiko la Hunt (ktj) tunaelezwa kuwa mwanafalsafa Aristotle alizaliwa mwaka 384 KM huko Ugiriki katika mji wa Stagira, uliokuwa na bandari wakati huo. Aristotle akiwa na umri wa miaka 17 alijiunga na Chuo cha Plato. Kama mwaka 338KM, mwanazuoni huyu alianza kazi ya ukufunzi katika Chuo cha Alexander Mkuu. Mwaka 335KM, Aristole alianzisha chuo chake huko Anthens, Ugiriki. Aristotle alitumia muda mwingi sana wa maisha yake kusoma, kufundisha na kuandika mambo mbalimbali ya kitaaluma akiwa katika chuo chake hicho. Mwanafalsafa huyu alichangia kwa sehemu kubwa sana katika elimu ya sayansi na falsafa. Mawazo na ugunduzi wake uliwachochea watu wengi kutafiti mambo mbalimbali. Pia inaaminika kuwa maandishi ya Aristotle yamesomwa na watu wengi sana ulimwenguni mpaka kufikia karne hii tuliyomo leo.

Aristostle alifariki mwaka 322KM miaka michache baada ya kuhama jiji kubwa la Ugiriki, Athens na kuelekea Chalcis huko huko Ugiriki (Hunt, 2021). Mwalimu mkuu wa Aristotle alikuwa Plato. Kwa kuwa zamani maarifa hayakusomwa kipwekepweke, mwanafalsafa huyu alisoma na kupata ujuzi katika mambo mbalimbali (Hunt, 2021). Aristotle alikuwa na ujuzi wa fani mbalimbali mathalani Sanaa (Muziki), Nyota, Biolojia, Maadili, Lugha (Isimu), Sheria, Fasihi (Tamthiliya na Ushairi) n.k.

Wamitila (2008) anaeleza kuwa katika uga wa fasihi, Aristotle amejitokeza katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza mawazo yake yamejikita kwenye chanzo ama chimbuko la fasihi ulimwenguni kwa jumla. Sehemu ya pili anajadili kuhusu fasihi (tanzu za fasihi; tamthiliya na ushairi pamoja na dhima za fasihi). Katika tamthiliya, Aristotle alijikita zaidi hasa katika utanzu wa tanzia (Wamitila, 2008). Aristotle aliandika kitabu kiitwachwo POETIC na katika kitabu hichi, Aristotle anaainisha vipengele sita vya tamthilia ya kitanzia (Mbogo, 2016). Vipengele hivyo ni hivi; Msuko [Mythos], Wahusika [Ethos], Dhamira [Theme], Matumizi ya lugha

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

[Lexis], Nyimbo [Melopocia] na Maonesho [Opsis].

Kwa mujibu wa Aristotle kuna aina mbili za tamthiliya (Mashele, 2020). Aina ya kwanza ni tamthiliya tanzia na aina ya pili ni tamthiliya ramsa. Tamthiliya tanzia ni tamthiliya ambayo hutumika kuonesha kuanguka na kushindwa kwa mhusika maarufu, mbabe au shujaa ambaye hutoka katika tabaka la juu, yaani mtu wa nasaba bora (Wamitila, 2003). Tanzia ya Kiaristotle ni usanii uoneshao anguko la mtu ambaye kimsingi ni mwema, shujaa na mbabe. Kutokana na kosa la kufisha au la uamuzi mbaya ambao matokeo yake ni mateso kwa shujaa, mhusika mkuu. Jambo hilo baya linapompata shujaa huyo, jamii nzima huingia katika woga na kuhangaika kwa hali ya juu. Katika makala haya tumemakinika na aina ya tamthiliya tanzia.

### Mihimili ya Nadharia ya Kiaristotle

Semzaba (1997) amebainisha mihimili mbalimbali ya nadharia ya kiaristotle akirejea mawazo ya mwanafalsafa huyo kuhusu tamthiliya tanzia. Semzaba (ktj) ameeleza mihimili msingi ambayo inapaswa kuitambulisha tamthiliya tanzia inayobuniwa kwa kuegema kwenye nadharia ya kiaristotle. Mihimili ya nadharia ya kiaristotle inayobainishwa na mwanazuoni huyo dhidi ya tamthiliya tanzia imeelezwa hapa chini katika sehemu inayofuata. Kwa mujibu wa nadharia ya kiaristotle tamthiliya tanzia yoyote inapaswa kuzingatia mihimili ifuatayo:

### Tanzia Sharti iwe Matendo na Malengo Dhati

Kwa mujibu wa Aristotle, tamthiliya tanzia ilipaswa kujumuisha matendo na malengo dhati. Aristotle aliuona utanzu huu kama mwigo au uigazi wa tendo ambalo lina udhati, ukamilifu, ubora, na ukuu wa namna fulani. Tendo hilo lazima liwe na uwezo wa kuwaathiri watazamaji na kuwafanya waingiwe na huzuni ama kihoro. Tendo hilo lilipaswa kuwa na uwezo wa kuzitakasa hisia za uoga au huzuni katika kile alichokiita: Mtakasohisia [Catharsio].

### Shujaa kutoka Tabaka la Nasaba Bora

Tanzia aliyoikusudia Aristotle ililenga wahusika wanaotoka tabaka lenye nasaba bora mathalani Mfalme, Malkia n.k. (Mbogo, 2016). Mhusika aliyepata mkasa katika tanzia ya kiaristotle ni lazima awe mwema na mwenye kuvutia kwa sura au kwa tabia au kwa uzuri. Wema au uzuri huu ndiyo huifanya hadhira kumpenda na hatimaye kusikia vibaya mtimani au kumwonea huruma mambo mabaya yanapomsibu.

### Watazamaji Huonyesha Kuumia kwa Yanayomsibu Mhusika Mkuu

Katika tamthiliya tanzia, hadhira wanapoitazama inapochezwa jukwaani huonyesha kusikitika kwa kadri shujaa, mtu mwema anapokabiliwa na mateso. Tanzia nzuri hupimwa kwa kigezo hiki, kutazama mrejesho wanaotoa hadhira katika igizo linalowasilishwa mbele yao hasa mwisho wa mchezo. Wanasanaa wanapopima kazi zao kuwa zimepokelewa vipi na hadhira, hutizama nyuso za hadhira yao (Mbogo, 2016). Katika tanzia hadhira huumia na kusikitika mno kwa kuona mtu asiye na hatia anakumbwa na mabaya wakati hakusitahili. Pengine kutokana na uzuri wake, hadhira ilitaraji mambo mema yamkute mhusika huyu, lakini huwa kinyume chake. Aristotle (1965) anauita huo 'Utakaso', kwamba hadhira akiguswa moyo, anaweza kubadilika na kuwa mtu mwema kutokana na mguso alioupata.

### Anguko la Shujaa Huchagizwa na Maamuzi Mabaya Anayofanya

Katika tamthiliya tanzia kwa mujibu wa Aristotle, anguko la shujaa huja kutokana na ama uamuzi wake mbaya au kosa lake mwenyewe. Aristotle aliona kuwa hakuna kosa la bahati mbaya katika maisha. Kila mkasa mbaya ni tokeo la maamuzi mabaya au kosa fulani lililofanywa na mhusika. Kwamba, shujaa huiona hatari iliyoko mbele yake katika hilo analokusudia kuliendea. Kukosea kwake katika kufanya maamuzi ndiko hupelekea akaja kuangukia kwenye janga.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**Muundo wa Tamthiliya Tanzia**

Kwa mujibu wa Aristotle tamthiliya (ya Kigiriki) ilipaswa kuwa na vipengele sita muhimu. Vipengele hivyo ndiyo vinaonekana kuzingatiwa katika utunzi wa tamthiliya ya kiaristotle. Vipengele hivyo ni; Msuko Wahusika, Dhamira/Fikra, Matumizi ya lugha, Nyimbo na Maonesho. Utunzi wa tanzia ya kiaristotle ulipaswa kuzingatia vipengele hivyo.

Kimsingi hii ndiyo mihimili inayoelezwa katika nadharia ya kiaristotle dhidi ya tamthiliya tanzia. Mihimili ya nadharia hii ilituongoza kuchambua mbinu za kiaristotle na zisizo za kiaristotle katika tamthiliya teule ya *Sadaka ya John Okello*.

**WASIFU WA EMMANUEL MBOGO NA MUHTASARI WA TAMTHILIYA TEULE**

Emmanuel Mbogo ni mtunzi na mwandishi wa tamthiliya, riwaya na hadithi fupi katika fasihi ya Kiswahili. Mtunzi huyu anaishi Dar es Salaam, Tanzania hapa Afrika Mashariki. Tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* tuliyoitumia katika makala haya imeandikwa na mtunzi huyo, Emmanul Mbogo. Mningo (2015) anammweleza Emmanul Mbogo kama mwanazuoni nguli katika uga wa sanaa za maonyesho na filamu katika fasihi ya Kiswahili. Emmanuel Mbogo alizaliwa tarehe 01/03/1947 katika wilaya ya Kongwa, mkoa wa Dodoma.

Emmanuel Mbogo alisoma katika Shule ya Msingi Mpwapwa na kuhitimu darasa la nane mwaka 1963. Baadaye alijiunga na masomo ya sekondari katika shule ya sekondari Indian (kwa sasa inajulikana kama Shule ya Sekondari Dodoma) na kuhitimu mwaka 1967. Mwaka 1968 alijiunga katika Chuo cha Ualimu Kigurunyembe, Mkoa wa Morogoro. Mwaka 1974 alijiunga na Chuo cha Elimu ya Taifa, Dar es Salaam kusomea Stashahada ya Sanaa za Maonyesho. Mwaka 1976 hadi 1979 alisoma Shahada ya Sanaa za Maonyesho, Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Mwaka 1981 alihitimu Shahada ya Uzamili ya Sanaa za Maonyesho hapo hapo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mwaka 1981-1985 aliendа kusoma Ujerumani, katika Chuo Kikuu cha Humboldt na kutunukiwa Shahada ya Uzamivu katika taaluma ya Sanaa za Maonyesho. Emmanuel Mbogo ni Profesa wa Sanaa za Maonyesho, Drama na Fasihi ya Kiswahili. Hadi anastaafu kufundisha mwaka 2020, alikuwa mhadhiri mwandamizi wa fani mbalimbali za filamu, sanaa za maonyesho na fasihi kwa ujumla Chuo Kikuu Huria cha Tanzania jijini Dar es Salaam (Mbogo, 2022).

Emmanul Mbogo, mtunzi teule katika makala haya, hata sasa ameshaandika na kuchapisha kazi mbalimbali za fasihi andishi ya Kiswahili; tamthiliya, riwaya pamoja na hadithi fupi. Tamthiliya alizokwisha tunga na kuzichapisha ni hizi zifuatazo; *Watoto Wetu* (1972), *Giza Limeingia* (1980), *Tone la Mwisho* (1981), *Morani* (1983), *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988), *Fumo Liyongo* (2009), *Sundiata* (2011), *Sadaka ya John Okello* (2015), *Nyerere na Safari ya Kanaani* (2015), *Wangari Maathai* (2015), *Nyota ya Tom Mboya* (2016), *Mondlane na Samora* (2016), *Malkia Bibi Titi Mohamed* (2016), *Ndoto za Josefu* (2016) n.k. Katika utanzu wa riwaya mwandishi huyu ameandika na kuchapisha kazi mbalimbali. Riwaya ambazo ameandika mtunzi huyu na kuzichapisha ni hizi zifuatazo; *Watoto wa Mama Ntilie* (2002), *Vipuli vya Figo* (2008) na *Siri za Maisha* (2010). Ndani ya riwaya hizi mfasihi huyu amezungumza mambo mengi yanayoihusu hasa jamii ya kitanzania katika nyuga mbalimbali za kimaisha mfano; uchumi, siasa na kiutamaduni. Katika makala haya tulichagua kutumia tamthiliya moja ya Emmanuel Mbogo, *Sadaka ya John Okello* (2015). Kwa hivyo mjadala wetu utajikita tu katika tamthiliya hii teule. Tulichagua tamthiliya hii kwa maksudi kabisa kwa sababu ndiyo ingeweza kutupatia data za makala haya kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na kazi nyingine alizoandika Emmanuel Mbogo.

*Sadaka ya John Okello* ni tamthiliya tanzia. Mtunzi wa tamthiliya hii ni mwandishi nguli katika sanaa za maonyesho na filamu hapa nchini Tanzania, Emmanuel Mbogo. Tamthiliya hiyo ilitungwa na kuchapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 2015, Dar es Salaam. Tamthiliya hii inaeleza kuhusu mapinduzi

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

yaliyofanyika Visiwani Zanzibar mnamo mwaka 1964, Januari 12. Mtunzi ameijenga tamthiliya hii tanzia katika maonyesho 12. Tamthiliya imeanza kwa sherehe za uhuru wa Zanzibar zilizofanyika Disemba 10, 1963 visiwani Zanzibar. Sherehe hizo za Uhuru wa Zanzibar zinafanyika chini ya Sultan Seyyid Jamshid. Jukwaa limepambwa lakini bado Bendera ya Wingereza inapepea. Upande mwingine, Bendera ya Zanzibar imekunjwa inasubiri ipepee ifikapo saa 6:01 usiku. Katika sherehe hizo za uhuru tunaonyeshwa baadhi ya Wazanzibar kutofurahishwa na dhuluma waliyofanyiwa. Muingereza kumuachia mamlaka mgeni, Muarab Sultan Seyyid Jamshid badala ya mtu mweusi, raia mzawa wa visiwa vya Zanzibar. John Okello na wenzake ni miongoni mwa watu weusi waliokasirika hata kuweka nia ya kupambana na dhuluma hiyo waliyotendewa na Wingereza.

John Okello akizungumza na wenzake; Ramadhani na Mfaranyaki siku moja baadaye baada ya sherehe za uhuru wa Zanzibar anaonyesha kukasirishwa na hotuba iliyotolewa na rais mpya wa Zanzibar, Sultan Jamshid. Okello anawaelekeza Wazanzibar kupambana hata kumwaga damu ili uhuru halisi wapewe Wazanzibar weusi, rais halisi visiwani humo si raia wageni, Waarab. Okello anaratibu mapambano kwa kupata vijana kwenda msituni kujiandaa kufanya mapinduzi ya kijeshi dhidi ya serikali ya Zanzibar. Okello ameongoza jeshi la vijana wenzake na hatimaye amefanikiwa kupata uhuru wa kweli, Januari 12, 1964. Baada ya Zanzibar kupata uhuru wa kweli kwa njia ya mapinduzi, Okello anasalitiwa na Wazanzibar. Wanainuka raia wengine wakimtaka Okello arudi kwao kwani naye si raia halisi wa Zanzibar bali ni raia wa Uganda. Okello anafukuzwa kutoka ardhi ya Zanzibar kwa dai kuwa si mzawa.

Kimsingi, *Sadaka ya John Okello* ni tamthiliya nzuri ya kihistoria. Tamthiliya hii inaeleza mengi kuhusu mapinduzi yaliyotukia Zanzibar mwaka wa 1964. Tamthiliya inaeleza hatua mbalimbali za ukombozi zilizochukuliwa tangu Zanzibar ipate uhuru kutoka kwa Waarabu Disemba 10, 1963. Mtunzi wa tamthiliya hii amesawiri matukio hayo akihusisha makundi mbalimbali yaliyojitokeza kupambana na Waarabu. Kundi la John Okello ndilo lililofanikiwa kufanya mapinduzi na kuikomboa Zanzibar. Mwishoni taifa limekuwa chini ya Wazanzibar, serikali ikiongozwa na Mzee Abeid Karume (1964 – 1972).

## Mbinu za Kiaristotle katika Tamthiliya ya Sadaka ya John Okello

Makala haya yamechambua kanuni au mbinu za kifani za Kiaristotle na zisizo za Kiaristotle ambazo zimetumika katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello*. Katika sehemu inayofuata hapa chini tumeonyesha mbinu na kanuni za kiaristotle zilizotumiwa katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello.* Tumetumia vipengele muhimu sita vilivyobainishwa na Aristotle, vinavyobainisha tamthiliya tanzia. Mihimili ya nadharia ya kiaristotle imetuongoza kufanya mjadala huu.

### *Msuko*

Wamitila (2008) anasema kwamba, "Msuko ni mfuatano wa matukio yanayopatikana katika fasihi kwa kutegemea uhusiano wake kiusababishi." Analoshadidia mwanazuoni huyu katika uga wa fasihi kuhusu dhana ya msuko ni hili, katika kazi ya fasihi tukio awali linapaswa kutengeneza njia ya tukio linalofuata katika fasihi. Ndiyo kusema, matukio hayo yakipangiliwa sawia, hukamilishana ili hufanikisha lengo la mtunzi. Kwamba, ni rahisi hadhira kuelewa kile kilichokusudiwa ama dhamira inayowasilishwa kwake kutokana na mpangilio mzuri wa matukio katika kazi husika.

Hali kadhalika dhana ya msuko katika kazi za fasihi hufasiliwa kama mtiririko wa vitushi katika kazi za fasihi (Bosibori, 2016). Mtafiti huyu anaendelea kudadavua kuwa, katika fasihi msanii huanza na kitendo cha kwanza na kuonyesha jinsi vitendo vinavyofuatana na kuathiriana hadi kufika tamati ya kazi yake. Hivyo, matukio yote yanayopangwa katika kazi za fasihi, hupangwa kiubunifu ili yakamilishane.

Kimsingi, msuko ni mpangilio wa matukio pamoja

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

ubainishaji wa vyanzo vyake katika kazi ya fasihi. Wamitila (2003) ameainisha misuko mbalimbali katika kazi za fasihi; msuko kinzani, msuko msago, msuko mkuu, msuko kioo na msuko rudufu. Ndiyo kusema, mtiririko wa vitushi, matukio katika kazi za fasihi unatofautiana, kwani kila mtunzi huchagua mtindo wa kutumia anapoamua kubuni kazi ya fasihi ili aiwasilishe kwa hadhira.

Mwanafalsafa Aristotle alikiona kipengele cha msuko kama kipengele cha lazima katika muundo wa tanzia. Mtaalam huyo anasema kwamba, tanzia lazima ioneshe umoja au mshikamano wa mandhari, muda, na matendo ili kuendeleza msuko inavyopasa. Msuko huo lazima udhihirike waziwazi ili msomaji au mtazamaji aweze kuutambua mapema. Msuko unapaswa kuwa wa mantiki na tarahuki. Vilevile msuko unafafanuliwa kwa namna nyingine kama mpango wa vitendo, matendo ambayo huwekwa kwenye mtiririko wa kufikia kilele, yaani kwamba, kitendo cha pili kinatokana na kitendo cha kwanza na kitendo cha nne kinatokana na kitendo cha tatu n.k (Bikorimana, 2020).

Sifa ya msuko tanzia inajitokeza katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello*. Tamthiliya hii imepangwa katika matendo kumi na mbili (12). Maonyesho hayo yapo katika hali ya kukamilishana. Kwa mfano, katika onyesho la kwanza, mtunzi ameonyesha namna Mkoloni, Mwingereza anavyokabidhi mamlaka kwa Sultan Jamshid Januari, 12, 1963. Tukio hili halipokelewi vema na Wazawa/Waafrika. Matendo yote yanayofuata yanaeleza mwitiko wa tukio hilo hadi kufikia Onyesho la 10, mapinduzi yanapofanyika na mwishoni katika onyesho la 11 na 12 tumeonyeshwa yaliyojiri punde tu baada ya mapinduzi hayo. Kwa hakika visa vimepangiliwa kwa namna nzuri. Msingi huu wa kiaristotle umezingatiwa barabara na mtunzi teule, Emmanuel Mbogo.

***Wahusika***

Bosibori (2016) anasema kuwa, mhusika ni mtendaji katika kazi ya fasihi na huwa kielelezo cha viumbe wanaopatikana ulimwenguni ingawa si lazima sifa zote za mhusika zifungamane moja kwa moja na sifa za mwanadamu. Mtafiti huyu anawatazama wahusika katika kazi za fasihi kama viumbe wanaotumiwa na msanii kuwasilisha mawazo yake. Viumbe wanaotajwa kuwa ndani ya kazi za fasihi wanaweza kuwa wanyama, ndege au binadamu. Namna yoyote ya mhusika anayetumiwa katika kazi za fasihi, hutumiwa kama taswira ya binadamu halisi katika jamii anayoilenga mtunzi wa kazi ya fasihi; fanani ama mwandishi kutegemea na kumbo anayotumia.

Njogu na Chimerah (1999, uk. 45) wanasema, “Wahusika ni sehemu ya fani na ni viumbe wa sanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii.” Wanazuoni hawa wanaendelea kutufahamisha kuwa, mazingira ya msanii yanaweza kuwa ya kijiografia, kihistoria, kitamaduni au kisiasa. Kimsingi, wanaloshadidia Njogu & Chimerah (khj) ni kwamba, viumbe wote wanaotumiwa na msanii katika kazi ya fasihi ndiyo huitwa wahusika. Namna ya kubuni wahusika hao huathiriwa na mazingira aliyomo msanii wa kazi mahsusi ya fasihi.

Kwa jumla, katika kazi za fasihi wahusika ni viumbe ambao hubebeshwa migongano au mvutano. Migongano hiyo kati yao ndiyo hupelekea kazi ya fasihi kusonga mbele. Viumbe hivyo mara nyingi vinabainishwa kama binadamu, wanyama, ndege, vitu n.k. Kuhusu dhana hii, mwanazuoni katika uga wa fasihi, Semzaba (1997) anasema kwamba, tamthiliya ni tawi mojawapo la fasihi andishi hutawaliwa na migongano baina ya wahusika ambayo huwekwa wazi, hukuzwa na kusuluhishwa. Migongano hii hudhihirika kwa maneno na matendo ya wahusika na huwasilishwa kwa hadhira kutokana na falsafa ya jamii au ya mtunzi mwenyewe.

Katika tanzia za kiaristotle, wahusika huwekwa katika pande mbili. Mosi, upande unaokubalika zaidi na jamii au hadhira. Pili, upande usiokubalika zaidi na hadhira au jamii. Katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello*, upande wa John Okello na wenzake au wanamapinduzi wenzake ndiyo unaokubalika na kupendwa kwa hayo wanayoyafanya. Upande wa pili

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

wa Sultan na vijana wake akina Rashid ndiyo usiokubalika, unafanya mambo mabaya ambayo jamii haiyataki. Mgongano baina ya makundi haya mawili umetambulishwa wazi katika kitendo cha kwanza, baada ya Gavana, Mkoloni kukabidhi madaraka kwa Sultan na kisha Mzee BABU kunyang'anya Maikrofoni na kuzungumza na umma kuwa hajaridhika na hicho kinachofanyika:

> *BABU: Nakwambieni: noti bandia na noti asilia zote ni pacha, lakini hazifanani.*
>
> *UMMATI: (Kelele, shangwe)*
>
> *BABU: Wazanzibar wenzangu,*
>
> *Mimi nauliza, mioyo ya walala hoi.*
>
> *Itaendelea kuvuja damu hadi lini? ... (Onesho la Kwanza, Uk. 5)*

Katika sehemu hii ya kwanza, mtunzi ametumia wahusika wake kuonesha mgogoro uliomo katika kazi yake. Kwamba mgogoro huo uliopo hapo ni wa kisiasa. Jamii imo katika mahitaji ya ukombozi wa kweli. Kwa hivyo kila muhusika aliyechorwa ama kuchopekwa katika tamthiliya hii amechorwa ili kuufikisha mgogoro huu hatma, suluhisho.

***Maonesho***

Hussein (1983) na Semzaba (1997) wanaeleza kuwa maonesho katika tanzia ya Kiaristotle huwekwa katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya mwanzo, kati na mwisho. Sehemu hizi tatu hutawaliwa na migongano baina ya wahusika. Katika sehemu ya kwanza, mgogoro huwekwa wazi. Pamoja nayo, sehemu ya pili mgogoro hukuzwa hatimaye sehemu ya tatu, mgogoro/mgongano husuluhishwa.

Katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello*, Sehemu ya kwanza imebebwa na Onesho la Kwanza, ambamo mtunzi ameutambulisha mgogoro unaoibuka kutokana na makabidhiano ya uhuru bandia baina ya Gavana wa Kiingereza na Sultan Jamshid ambaye si mzawa wa visiwa hivyo. Tukio hilo ndilo limeibusha fikra na hali za kupambana ndani ya vijana wa Kiafrika, John Okello akiwa sambamba na vyama vya upinzani vya siasa ili kupambana na udhalimu huo waliofanyiwa na watu kutoka Ulaya.

Sehemu ya pili inabebwa na onesho la pili hadi la tisa ambapo mgongano unakuzwa. Harakati zote za kufanyika kwa mapinduzi na mipango mbalimbali imezungumzwa katika maonesho hayo. Kwa mfano: Mazoezi ya Kijeshi yanafanyika katika Onesho la Tano chini ya uongozi wa Field Marshall John Okello (uk. 22). Vijana mbalimbali wa Kiafrika wanashiriki mazoezi hayo. Miongoni mwao ni Ramadhani Haji, Seif Bakari, Iddi, Mohammed, Absolom Amoi, Mathias Simba n.k.

Sehemu ya tatu ni mshuko na suluhu ya mgongano huo inapatikana. Hapa kuna onyesho la kumi hadi la kumi na mbili. Kwa mujibu wa Aristotle sehemu ya tatu ndiyo huonyesha suluhu ya mgongano ulioibuliwa katika sehemu ya kwanza. Tamthiliya *Sadaka ya John Okello* inatii kanuni hii na kwa hakika inaoneka waziwazi kwa wasomaji na wahakiki wake. Onesho la kumi ndipo mapinduzi yanafanyika na visiwa vya Zanzibar vinanyang'anywa kutoka katika himaya ya Waarabu, Masultani, ambao wanatoroka punde tu baada ya kujua kuwa Ikulu yao imevamiwa na kupinduliwa (Onesho la Tisa).

***Matumizi ya Nyimbo na Lugha ya Kishairi***

Wamitila (2008) anasema, "Sifa moja inayotokeza kwa mapana sana katika tamthiliya nyingi ni matumizi ya lugha ya kishairi." Mwanazuoni huyu anazidi kushadidia kuwa, matumizi ya mtindo huu humlenga zaidi msomaji, hadhira na si wahusika katika drama husika. Lugha ya kishairi huwa msingi muhimu wa kutoa mawazo yenye uhisivu fulani na uhusishwa zaidi na mambo au mada zenye mhemko na hisia nzito.

Kimsingi hii pia ni mojawapo ya sifa kuu inayotakiwa katika drama tanzia ya kiaristotle. Katika tamthiliya hii ya *Sadaka ya John Okello* kanuni hii imejitokeza. Mtunzi ametumia nyimbo pamoja na lugha ya kishairi katika maonyesho

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

mbalimbali. Kwa mfano Wimbo wa Taifa la Uingereza katika ukurasa wa 2, onyesho la kwanza. Umeandikwa na kunukuliwa kwa ukamilifu. Wimbo huu una beti sita (6). Hapa chini tumenukuu ubeti wa kwanza,

> *"God save our gracious Queen!*
>
> *Long live our noble Queen!*
>
> *God save the Queen!* (Onesho la Kwanza, Uk. 2)

Lugha ya kishairi pia imetumika sehemu mbalimbali na mwandishi wa tamthiliya hii ya *Sadaka ya John Okello*, Profesa Emmanuel Mbogo. Tutizame mfano huu;

> *ZIMWI 2: Okello! Okello, umefuata nini visiwani?*
>
> *Hapa visiwani hakuna Msalaba*
>
> *Hapa Zanzibar tunatazama Kibla*
>
> *Hatutazami Golgota. (Onesho la Kumi, Uk. 35)*

Matumizi ya utanzu wa ushairi na kaida zake ni ithibati nyingine iliyotumika kuthibitisha sifa za tamthiliya za kiaristotle katika tamthiliya teule tuliyotalii katika makala haya. Emmanuel Mbogo ametumia fani hii barabara kama inavyotumika katika drama za kiaristotle tangu kale wanazuoni wa kiaristotle walipoasisi mihimili hiyo. Kwamba, tamthiliya ya kiaristotle iwe na utambulisho gani.

### *Matumizi ya Lugha*

Hapa kinachosisitizwa zaidi ni matumizi ya lugha katika tamthiliya ya Kiaristotle. Katika tanzia za kiaristotle, wahusika hupewa maneno au uzungumzi kutokana na uhusika wao, nafasi wanayoiigiza (Mhando, 2015). Kwamba, uzungumzi wa mhusika mfalme ni tofauti na uzungumzi wa mhusika wa kawaida kutoka tabaka la chini. Sifa hii inaonekana katika tanzia ya *Sadaka ya John Okello*. Kwa mfano, namna Gavana wa Uingereza anapozungumza mbele ya hadhara akihutubia mara ya mwisho, maneno yamepangiliwa vema. Maneno yamebuniwa kuendana na tukio linalotendeka, mandhari na hadhira husika. Ndani ya hotuba hiyo kuna maneno mengi ya heshima, ya kufurahisha, kwamba mpaka hadhira iliyokaa kuyasikiliza inayafurahia. Tutizame lugha ya Gavana. Maneno yake yameteuliwa na kupambwa vema. Yameenda na nafasi ya uhusika wake katika tanzia hii. Taz.

> ***GAVANA****: Usiku huu ni usiku wa fumbo la kihistoria*
>
> *Historia iliyofumbata ua la alizeti, ua la waridi,*
>
> *Ukitaka!* .. (Onesho la Kwanza, Uk.1)

Emmanuel Mbogo amejitahidi kuwapa wahusika maneno, matamshi yanayoendana nafasi wanazocheza kwenye tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello.* Mathalani mhusika Gavana, kiongozi wa kisiasa au utawala kwenye ngazi mbalimbali katika nchi ama taasisi amepewa maneno yanayoendana na uhusika wake. Mtunzi ametumia maneno yenye taswira ya mamlaka ndani yake. Mhusika huyu anazungumza kwa ujasiri mkubwa mbele za watu. Hali inayosawiri watu wenye mamlaka wanapozungumza mbele ya watu wanaowatala.

### *Dhamira/Fikra*

Mwanafalsafa wa Kigiriki, Aristotle anaona kwamba, kazi yoyote ya kifasihi, sharti iwe na dhima fulani. Mtanzia huyu aona kuwa fasihi si ya kuburudisha pekee bali mtunzi hubeba wazo fulani ama fikra aitakayo kuifikisha kwa jamii yake anayoiandikia (Wamitila, 2008). Aristotle anaendelea kueleza kwamba, mtunzi huonyesha dhamira zake au fikra zake kupitia matamshi, lugha anayowabebesha wahusika wake. Pia anaweza kuonyesha mawazo fulani aliyonayo kupitia mabishano au mazungumzo baina ya wahusika wake.

Ndani ya mazungumzo, matamshi, misuguano baina ya wahusika ndimo tunaweza kupata dhamira mbalimbali za mtunzi. Katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* kuna dhamira mbalimbali zimeibuliwa. Kwa mfano; ukombozi wa kweli,

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

ukoloni mamboleo, matabaka katika jamii, mapenzi na ndoa, ushujaa, usaliti n.k. Mhusika mkuu John Okello amechorwa na mwandishi kujadili dhamira ya usaliti katika jamii. Pamoja na jitihada kubwa anazofanya ndugu huyu, maisha yake yanaishia Gerezani. Kisha watu ambao hawakuhusika hata kidogo katika kufanya mapinduzi hayo ndiyo wanakula na kuifadi Keki ya Mapinduzi. Emmanuel Mbogo anaonyesha kuwa usaliti katika jamii upo na siyo mzuri. Ni vema jamii ikaepukana nao kila inapobidi. Historia inaonyesha kwamba, John Okello, raia kutoka nchini Uganda alishiriki kwa kiwango kikubwa sana katika kuleta mapinduzi nchini Zanzibar, Kisiwa cha Unguja. Mapinduzi yalifanikiwa, sawa! Mgeni Sultan akasalenda, akakubali yaishe na kukabidhi madaraka kwa wazawa. Okello badala ya kushiriki zawadi ya mapinduzi akaishia kufungwa Gerezani. Mbogo anafananisha jitihada za John Okello na Sadaka[1] anayotoa mtu kanisani.

**Mbinu Zisizo za Kiaristotle katika Tamthiliya *Sadaka ya John Okello***

Tumeona hapo awali kuwa tamthiliya hii ni drama tanzia, hata hivyo imejumuisha baadhi ya misingi isiyo ya kiaristotle. Katika hii sehemu pili tumeonyesha misingi na mbinu zisizo za kiaristotle zilizotumika katika tamthiliya hii teule, *Sadaka ya John Okello.*

***Mbinu ya Monolojia***

Kietimolojia, monolojia ni neno la Kigiriki lenye maneno ‘monos’ lenye maana ya peke yake na ‘logos’ lenye maana ya uneni (Sanga, 2018). Mtafiti huyu anaendelea kudadavua dhana ya monolojia kama mbinu ya kifasihi itumiwayo kuwasilisha usemaji wa ndani wa mhusika wa kazi za fasihi katika kuwasilisha mawazo na hisia zake kwa sauti. Wakati mwingine mhusika huzungumza moja kwa moja na hadhira au mhusika mwingine. Sanga (khj) akimrejea Bakhtin (1981) anabainisha kuwa, mbinu ya monolojia hutumiwa zaidi katika utanzu wa drama (maigizo na filamu) na ushairi.

Kimsingi, monolojia ni usemaji nafsi au usimulizi nafsi. Katika mbinu hii mhusika huongea peke yake. Tunaweza kusema, huwaza kwa sauti. Mawazo yake nafsini huwekwa nje kama anazungumza. Katika tanzia ya kiaristotle mbinu hii haitumiki. Katika tamthiliya *Sadaka ya John Okello*, mbinu hii imejitokeza. Mfano mzuri uko katika Onesho la Kumi na Mbili (12) ukurasa wa 66. John Okello anazungumza mwenyewe akiwa gerezani, Kamiti Prison.

> ***OKELLO:*** *[KIMYA]*
>
> *Kamiti Prison. Kosa langu nini? “Okello ameingia nchini Kenya kinyemela!”*
>
> *(anacheka kidogo) …*
>
> *Aa! Mfungwa hachagui jela. Karatasi za kuchambia hakuna. Maji ya kustanji vilevile*
>
> *hakuna…* (Onesho la Kumi na Mbili, Uk. 66.)

Kwa jumla, mbinu hii imetufaa kushadidia hoja kwamba, mtunzi teule wa tamthiliya hizi, Emmanuel Mbogo ametumia mbinu nyingine zisizo za kiaristotle katika kubuni kazi hii ya kidrama katika fasihi ya Kiswahili.

***Mbinu ya Majigambo***

Clemence (2015, uk. 29) anasema kuwa, “Majigambo ni mbinu ya kisanaa ya kusimulia na kujikweza kwa mtu kuhusu matendo na mambo muhimu ya kishujaa na kishupavu aliyoyafanya kwa uwezo wake au kwa nasaba yake.” Mtafiti huyu anaendelea kusema kwamba, masimulizi hayo hutolewa kwa njia ya kishairi na huambatanishwa na vitendo vya mjigambaji. Mjigambi huyo hudhihirisha aliyoyafanya huku akiwa amevaa maleba maalum pamoja na zana zinazoshadidia ushujaa wake.

[1] Sadaka ni kitu chochote kinachotolewa bure;msaada (BAKITA, 2022)

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

Seni (2020) akimrejea Mulokozi (1996, uk. 81) anasema, "Majigambo ni ghani za kujisifia. Kwa kawaida hutungwa na kughanwa na mhusika mwenyewe." Mulokozi (khj) anaendelea kueleza kuwa, jigambo hutungwa kwa ustadi mkubwa kwa kutumia mbinu kama sitiari, vidokezi, ishara, takriri na wakati mwingine hata vina. Kimsingi, wanazuoni hawa wametufaa kwamba, katika fasihi majigambo ni masimulizi ya kujisifu anayotoa mtu kuhusu mambo ya kishujaa aliyowahi kufanya katika maisha yake. Mtindo wa kishairi ndiyo unaelezwa kutumiwa zaidi na wajigambi katika kuwasilisha bunilizi zao.

Hivyo, tunaweza kuhitimisha kwamba majigambo ni masimulizi ya kujisifu kwa mtu kuhusu mambo ya kishujaa aliyowahi kufanya katika maisha yake. Wakati wa uwasilishaji wa majigambo, mhusika hutumia lugha ya kishairi pia hujumuisha vitendo mbalimbali kuakisi ushujaa huo. Vilevile mwasilishaji hudhihirisha aliyowahi kutafanya huku akiwa amevaa maleba maalum kuendana na ushujaa unaozungumziwa.

Mtunzi wa drama hii tanzia, Emmanuel Mbogo ametumia mbinu hii majigambo katika kazi yake hii ya *Sadaka ya John Okello*. Katika tamthiliya teule mbinu hii imetumika zaidi wakati wa maandalizi ya jeshi la mapinduzi. Field Marshall, John Okello pamoja na vijana wake IDDI na MFARANYAKI uk.23, Onyesho la Tano wamejigamba sana hapo wawapo uwanja wa mazoezi wakijiandaa kwa mapinduzi. Kwa mfano:

> *IDDI: Field Marshall John Okello*
>
> *Mimi shujaa Iddi.*
>
> *Ninaranda, ninatamba, ninatanda…* (Onesho la Nne, uk. 22)

Tunaposoma jigambo hili tunabaini mambo mengi magumu aliyowahi kupambana nayo Iddi tangu kuzaliwa hadi hapo alipofika kiumri. Iddi anapomaliza kujisifu, kujikweza, kujitambulisha kwa wenzake ili aonekane alivyo shujaa na hodari wenzake nao wanafanya vivyo hivyo. Waliojigamba katika onesho hili wengine ni MFARANYAKI na Field Marshall, JOHN OKELLO. Ndiyo kusema, mtunzi ametumia mbinu hii isiyo ya Kiaristotle katika kubuni drama tanzia ya Sadaka ya John Okello kuhusu mapinduzi ya Zanzibar, mwaka 1964.

### *Mbinu ya Kuchanganya Nathari na Ushairi*

Tamthiliya ya Kiaristotle hutumia lugha ya kishairi tu. Lakini sasa kutokana na mikondo mbalimbali iliyopitia hata sasa, waandishi wa tamthiliya zama hizi wanatumia ama kuchanganya pamoja mtindo wa kishairi na mtindo wa kinathari katika kazi zao. Mwandishi Emmanuel Mbogo katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* ametumia mitindo yote hii miwili. Mtindo wa kishairi hutumia lugha ya mkato ilhali mtindo wa kinathari hutumia lugha ya mjazo. Mfano mzuri unaonekana kupitia mhusika RASHIDI ukurasa wa kumi na tatu (13).

> *RASHIDI: Sikilizeni: Serikali ya Sultani Jamshid na Shamte iko imara.*
>
> *Haitishwi na ukomunisti wenu.*
>
> *Fauka ya hayo, vyama vyenu vya ASP na Umma Party tutavipiga kalamu, tuviuwe!*
>
> *Na mkizidi kudinda, serikali ya Sultani itawapiga kwa pigo la kudumu.*
>
> *(Anamgeukia Babu) Ati Babu!*
>
> *Wewe ni Babu ama babuni?*
>
> *Ama ni Bamboo; tete tupu lisilojaa nyama*
>
> *Au*
>
> *Ni Babu kababuka Kapanda mti kaanguka? … (Onesho la Pili, Uk. 13)*

Matumizi ya mitindo hii miwili mtawalia; nathari na ushairi katika tamthiliya teule si kaida ya drama za kiaristotle. Wanazuoni katika uga wa fasihi ya Kiswahili, Emmanuel Mbogo akiwa miongoni mwao wanaibua umbo lingine la drama ambalo hapo awali halikutumika watunzi wanapobuni tamthiliya kwa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

mhimili wa Aristotle.

***Mbinu ya Dayalojia***

Clemence (2015) anafasili dayolojia kama mazungumzo ya wahusika katika tamthiliya. Dialojia huwa na maneno machache yaliyoteuliwa vizuri ili kuisogeza mbele hadithi au kudhihirisha jambo alilokusudia mtunzi. Mbinu hii hutumika zaidi katika drama au tendi. Kupitia mtafiti huyu tunabaini kuwa, dayalojia ni mtindo wa mazungumzo ya wahusika ndani ya drama ambayo huwekwa katika hali ya kupokezana, mhusika huyu anaongea na mwingine anaitika. Mtindo huu upo katika mfumo wa majibizano. Tanzu za drama na tendi ndiyo hutumia zaidi mtindo huu katika bunilizi zake.

Katika drama tanzia za kiaristotle mbinu ya dayalojia haitumiki, pengine sasa katika mikondo iliyofuata baada ya ule wa mwanzo kabisa aliouasisi Aristotle. Wahusika katika drama hii ya *Sadaka ya John Okello* wanazungumza kwa kupokezana na mazungumzo yao kwa kiasi kikubwa yamewekwa na kupangiliwa kidayalojia. Kwa mfano;

*RASHIDI: Unguja na Pemba_Oyeeee!*

*UMMATI: Oyeeee!*

*RASHIDI: Abedi Amani Karume-Oyeeee!*

*UMMATI: Oyeeee! (Onyesho la Kwanza, Uk. 1)*

Tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello* ina wahusika wasiopungua thelathini. Kila mhusika amepangwa na kupewa pahala pa kuongea, kujibizana kutokana na uhusika wake na sehemu anayoiwakilisha. Mtindo huu si wa kiaristotle ingawa mtunzi ameutumia.

**HITIMISHO**

Kwa jumla, makala haya yamechambua mbinu za kiaristotle na zisizo za kiaristotle katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello.* Mtunzi teule, Emmanuel Mbogo ametumia mbinu za kiaristotle katika bunilizi hii. Hata hivyo mbinu zisizo za Kiaristotle zimetumika kushajiisha tamthiliya teule kama tulivyobainisha katikka makala haya. Vilevile tumebaini kwamba nadharia ya kiaristotle imepitia mabadiliko mbalimbali. Mathalani mhusika mkuu, shujaa katika bunilizi za kifasihi kwa mujibu wa nadharia hii zama hizi si lazima tena kutoka familia ya tabaka la juu au tabaka la kitawala, la kifalme. Mhusika sasa anaweza kutoka katika tabaka lolote katika jamii kama ilivyokuwa kwa John Okello, raia kutoka nchini Uganda. Matumizi ya nguvu za miungu nayo yamepungua sasa katika drama tanzia, zilizoegema katika nadharia ya kiaristotle tofauti na ilivyokuwa hapo kwanza wakati utanzu huu ulipoasisiwa huko Ugiriki na Mwanafalsafa Aristotle.

**MAREJELEO**


Aristotle, N. (1965). *Introduction to Aristotle (1965-02-01)*. Mc Graw - Hill Education.

Awhida, H. H. H. (2021). Matumizi ya Lugha katika Tamthiliya ya Sadaka ya John Okello. *Journal of Human Sciences 20 (1)*.

BAKITA (2022). *Kamusi Kuu ya Kiswahili (Toleo la 3)*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers Plc. Tanzania

Bikorimana, D. (2020). Uhakiki wa Fasihi. https://www.academia.edu/41870699/UHAKIKI_WA_FASIHI_1_.

Bosibori, B. T. (2016). *Mwingilianomatini katika Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Mstahiki Meya*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Autolitho Ltd.

Clemence, S. M. (2015). *Kuchunguza Mbinu za Tanzia za Kiaristotle katika Tamthiliya za Fumo Liyongo na Sundiata*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Hunt, F. (2021). Michango 10 ya Aristotle kwa Sayansi na Utamaduni (https://sw.warbletoncouncil.org/aportaciones-aristoteles-15015) .

Hussein, E. (1983). Hatua Mbalimbali za Kubuni na Kutunga Testo Teatrale Kufuatana na Misingi ya Kiaristotle (Uk. 197 – 205). *Makala za Semina za Kimataifa III*. Dar es Salaam. Taasisi ya Ukuzaji Kiswahili (TUKI).

Mashele, (2020). Tamthiliya ya Kiswahili https://www.masshele.co.tz/2020/01/tamthiliya-tamthiliya-ya-kiswahili.html.

Mbogo, E. (2015), *Sadaka ya John Okello*. Dar es Salaam: Karljamer Print technology.

Mbogo, E. (2016). *Tamthiliya ya Kiswahili (OSW 602)*. Dar es Salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mbogo, E. (2022). Wasifu wa Maisha yangu. Usaili Uwandani. Dar es Salaam.

Omar, M. (2019). *Sanaa za Maonyesho katika Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Omar, M. (2020). *Tamthiliya ya Kiswahili*. Dar es Salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Mhando, P. & Balisidya, N. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*. Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.

Mhando, R. E. (2015). *Kuchunguza Dhamira za Kijamii katika Tamthiliya ya Hatia ya Penina Mlama.* Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Dar es Salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi, M. M. (1996) *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Vyuoni na Vyuo Vyuo Vikuu (Toleo II)*. Dar es Salaam. Kauttu Publishers.

Mningo, R. A. (2015). *Tathmini ya Mwingilianomatini katika Utunzi wa Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya ya Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liyongo.* Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Dar es Salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Msangi, E. O. (2018). *Kuchunguza Ubiblia katika Tamthiliya za Emmanuel Mbogo*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Dar es Salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Njogu, K. & Chimerah, R. (2011). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu (Chapa 3)*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Ochieng, D. (2020). *Michakato ya Utafiti wa Isimu ya Kiswahili.* Dar es Salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Ponera, A. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu*. Dodoma. Central Tanganyika Press.

Sanga, A. (2018). *Mkengeuko wa Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi Fupi Andishi za Kiswahili: Mifano kutoka Magazeti ya Habari Leo, Nipashe na Mwananchi*. Tasnifu ya Uzamivu. Chuo Kikuu cha Dodoma.

Semzaba, E. (1996). *Tamthiliya ya Kiswahili.* Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Seni, D. J. (2020). *Fasihi Andishi* (Mhadhara Darasani). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Wafula na wenzake (2020). Uchanganuzi wa Miundo ya Aristotle katika Tamthiliya ya Kinjeketile. *Mulika V-39* (79 – 95). Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi.* Nairobi. Focus Publications

Wamitila, K. W (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi na Fasihi.* Nairobi. Vide ¬ Muwa Publisherw Limited.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

Zelda, E. (2022). *Mbinu za Utafiti katika Lugha ya Kiswahili*. Dar es Salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.